# NISHATI

HABARI ZA NISHATI

# News Bulletin

www.nishati.go.tz | Wizara ya Nishati | wizara_ya_nishati_tanzania | @Nishati2017 | Wizara ya Nishati

**Toleo Namba 36** **Machi 1 - 31, 2022**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA NISHATI**

Telegramu "NISHATI".
Simu: (255)-26-2322018
Nukshi: (255)-26-2320148
Barua Pepe: ps@nishati.go.tz

Mji wa Serikali -Mtumba,
Mtaa wa Nishati,
S. L. P. 2494,
**DODOMA**.


**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Kutokana na kuendelea kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia kunakosababishwa na mambo mbalimbali ikiwemo vita kati ya Urusi na Ukraine, mwenendo wa bei za mafuta nchini umeathirika kwa bei hizo kuendelea kupanda.

Katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali kupitia Wizara ya Nishati imeondoa **Tozo ya Shilingi 100 kwa kila lita** ya Dizeli, Petroli na Mafuta ya Taa, zilizopaswa kulipwa na watumiaji wa mafuta nchini kwa muda wa **miezi mitatu** zaidi kuanzia mwezi Machi 2022 hadi Mwezi Mei 2022 huku ikiendelea kutathmini mwenendo wa bei za mafuta katika soko la dunia.

Pamoja na kwamba uamuzi huu utaipunguzia Serikali mapato ya kiasi cha **Shilingi bilioni 30** kwa mwezi, Serikali imeona ni muhimu kuendelea kuwalinda wananchi wake dhidi ya athari za mabadiliko ya bei za mafuta ulimwenguni. Hii inatokana na ukweli kwamba endapo uamuzi huu usingechukuliwa na Serikali, bei za mafuta nchini kuanzia mwezi Machi na kuendelea zingekuwa za juu sana kutokana na sababu zilizoelezwa hapo juu.

Kwa msingi huo, **Mheshimiwa January Makamba (Mb), Waziri wa Nishati,** ameidhinisha na kusaini marekebisho ya kanuni inayohusika na Tozo hiyo ili kutimiza uamuzi huu wa Serikali.

Uamuzi huu unaenda sambamba na maelekezo ya **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** aliyoyatoa baada ya kikao na Wizara na taasisi mbalimbali zinazohusika na suala hilo zilizokutana tarehe 5 Oktoba 2021 kujadiliana namna bora ya kupunguza bei za mafuta hapa nchini na kupunguza tozo mbalimbali zenye thamani ya **Shilingi bilioni 102** kwa watumiaji wa mafuta nchini

Bei mpya za mafuta zitakazotangazwa na EWURA na kuanza kutumika tarehe 2 Machi 2022 zitazingatia marekebisho hayo ya kanuni yaliyofanywa na Waziri wa Nishati.

**IMETOLEWA NA:**

**WIZARA YA NISHATI**
28.02.2022

## HATI ZA MAKUBALIANO YA USHIRIKIANO WA MAFUTA NA GESI ASILIA ZASAINIWA ZANZIBAR








**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI**

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au
**Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma**




# BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
**Mhandisi Felchesmi Mramba**
Katibu Mkuu

**Makamu Mwenyekiti**
**Kheri Mahimbali**

**Mhariri**
**Dorina G. Makaya**

**Waandishi**

Teresia Mhagama
Zuena Msuya
Hafsa Omar
Timotheo Mathayo

**Msanifu Kurasa**

Lucas Gordon

**Wasiliana nasi kwa simu namba** +255-26-2322018
**Nukushi:** +255-26-2320148
au

**Fika Ofisi ya Mawasiliano**
Mitumba Dodoma,
S.L.P 2494, Dodoma





*www.nishati.go.tz*
*Wizara ya Nishati*
*@Nishati2017*
*wizara_ya_nishati_tanzania*
*Wizara ya Nishati*

# HATI ZA MAKUBALIANO YA USHIRIKIANO WA MAFUTA NA GESI ASILIA ZASAINIWA ZANZIBAR



*Viongozi mbalimbali kutoka Tanzania Bara na Zanzibar waliohudhuria hafla ya kusaini Hati za Makubaliano ya ushirikiano katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia kwa Taasisi zinazoshughulikia sekta hiyo (waliokaa), wakiwa katika picha ya pamoja na Wakuu wa Taasisi zilizosaini Makubaliano hayo. Wa pili kulia waliokaa ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini Dkt. Mngereza Miraji Mzee (wa pili kushoto), Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (wa kwanza kushoto), Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Rashid Msaraka (alimwakilisha Mkuu wa Mkoa),katikati na Meya wa Jiji la Zanzibar, Mahmoud Mussa (wa kwanza kulia). Hafla ya utiaji saini ilifanyika katika Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar*

**Na Teresia Mhagama**

Hati za Makubaliano ya ushirikiano katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia kwa Taasisi zinazoshughulika sekta hiyo kutoka Tanzania Bara na Zanzibar zimesainiwa na hivyo kufanya ushirikiano huo kuwa rasmi.

Hafla ya utiaji saini hati hizo za Makubaliano ilifanyika tarehe 19 Februari, 2022 katika Mkoa wa Mjini Magharibi na kushuhudiwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini Dkt. Mngereza Miraji Mzee, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali, Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Rashid Msaraka ((alimwakilisha Mkuu wa Mkoa) na Meya wa Jiji la Zanzibar, Mahmoud Mussa.

Viongozi wengine waliohudhuria Hafla hiyo ni Wakuu wa Taasisi zinazosimamia Sekta ya Mafuta na Gesi kutoka Tanzania Bara na Zanzibar pamoja wenyeviti wa Bodi za Taasisi hizo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dkt. Mngereza Miraji Mzee, alitaja Taasisi zilizosaini makubaliano hayo kuwa ni Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC), Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) na Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA).

Alisema kuwa, TPDC na ZPDC zitashirikiana katika maeneo mbalimbali ikiwemo kujenga uwezo kwa wataalamu ikiwa ni pamoja na kubadilishana wataalamu, vifaa na teknolojia katika masuala yanayohusu utafutaji Mafuta na Gesi asilia katika pande mbili za muungano, kubadilishana uzoefu katika kuchakata, kutafsiri na kutunza takwimu na taarifa mbalimbali zinazohusu utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa rasilimali ya mafuta na gesi asilia.

# HATI ZA MAKUBALIANO YA USHIRIKIANO WA MAFUTA NA GESI ASILIA ZASAINIWA ZANZIBAR

Alitaja baadhi ya makubaliano ya ushirikiano kati ya PURA na ZPRA kuwa ni kubadilishana uzoefu katika kuandaa na kutunga miongozo na kanuni mbalimbali zitakazosimamia shughuli za mkondo wa juu wa petroli; kuongeza ujuzi katika kufanya kaguzi za Mikataba ya Ugawanaji Mapato, kubadilishana uzoefu katika kusimamia utunzaji wa taarifa mbalimbali zinazohusu utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa rasilimali ya mafuta na gesi asilia na kushirikiana katika maeneo mengine ya ushirikiano katika eneo la mkondo wa juu wa petrol.

Aidha alisema kuwa, EWURA na ZURA zitashirikiana katika maeneo mbalimbali ikiwemo kutoa ushauri wa kitaalamu wakati wa kutayarisha nyenzo za kiudhibiti, kubadilishana uzoefu wa kiudhibiti katika maeneo ya kiufundi na kiuchumi katika sekta za Nishati na Maji ikiwemo ukokotoaji/ uandaaji wa bei/gharama za huduma na utekelezaji wake na kusaidiana katika masuala ya kiutawala, teknolojia na vitendea kazi pale panapohitajika.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Rashid Msaraka ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi alisema kuwa, utiaji saini wa makubaliano hayo ni matokeo ya juhudi kubwa zinazofanywa na viongozi Wakuu wa pande zote mbili za Muungano pamoja na Mawaziri wanaosimamia sekta hizo ambao wameonyesha umakini katika kusimamia sekta.



*Viongozi mbalimbali kutoka Tanzania Bara na Zanzibar waliohudhuria hafla ya kusaini Hati za Makubaliano ya ushirikiano katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia kwa Taasisi zinazoshughulikia sekta hiyo (waliokaa), wakiwa katika picha ya pamoja na Wenyeviti wa Bodi za Taasisi zilizosaini Makubaliano hayo. Wa Tatu kulia waliokaa ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini Dkt. Mngereza Miraji Mzee (wa pili kushoto), Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (wa kwanza kushoto), Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Rashid Msaraka (alimwakilisha Mkuu wa Mkoa) katikati na Meya wa Jiji la Zanzibar, Mahmoud Mussa (wa Pili kulia). Wa kwanza kulia ni Kamishna wa Petroli na Gesi, Michael Mjinja.*

Alisema kuwa, Taasisi hizo zimekuwa zikishirikiana kwa muda mrefu lakini sasa imekuwa rasmi kwenye maandishi na ni ishara ya kuendelea kutekeleza ushirikiano uliopo kwa umakini, ukaribu na mafahamiano ya karibu zaidi.

Alieleza kuwa, Taasisi hizo ni za kimkakati kwenye uchumi wa pande mbili za Muungano na hivyo alisisitiza kuwa ukaribu na mafahamiano yao yaendelee kwani yataleta mafanikio makubwa.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba alisema kuwa, jambo hilo la kutia saini makubaliano ya ushirikiano katika Mafuta na Gesi Asilia lina lengo la kuboresha na kuimarisha shughuli za utafiti wa mafuta na Gesi na kwa Tanzania Bara na Zanzibar na kwa Tanzania Bara tayari Gesi imegundulika ya kiasi cha futi za ujazo zaidi ya trilioni 57 na bado kuna dalili za upatikanaji mafuta.

Kutokana na makubaliano hayo rasmi ya ushirikiano, alizipongeza Taasisi hizo kwa kufikia maamuzi hayo ambayo yatafanya malengo ya Serikali ya kuendeleza rasilimali za Mafuta na Gesi Asilia kufanyika kwa haraka na kuweza kufikia mafanikio kwa muda mfupi zaidi.

# HATI ZA MAKUBALIANO YA USHIRIKIANO WA MAFUTA NA GESI ASILIA ZASAINIWA ZANZIBAR




*Wataalam mbalimbali kutoka Tanzania Bara na Zanzibar wakiwa katika hafla ya kusaini Hati za Makubaliano ya ushirikiano katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia kwa Taasisi zinazoshughulikia sekta hiyo. Hafla ya utiaji saini ilifanyika katika Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar*



*Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), Mhandisi Charles Sangweni (kulia) na Mkurugenzi Mwendeshaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA), Adam Abdulla Makame (kushoto) wakisaini Hati za Makubaliano ya ushirikiano katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia. Hafla ya utiaji saini ilifanyika katika Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar.*



*Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dkt. James Mataragio (kulia) na Mkurugenzi Mwendeshaji wa Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar, Mikidad Alli Rashid (kushoto) wakisaini Hati za Makubaliano ya ushirikiano katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia. Hafla ya utiaji saini ilifanyika katika Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar.*



*Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Mhandisi Godfrey Chibulunje (kulia) na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Bihindi Nassor Khatib (kushoto) wakipongezana mara baada kusaini Hati za Makubaliano ya ushirikiano katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia. Hafla ya utiaji saini ilifanyika katika Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar.*

# Serikali yakusudia umeme uwafikie wengi vijijini



Waziri wa Nishati, January Makamba

**Na Timotheo Mathayo, Dodoma.**

Serikali inakusudia kusambaza umeme vijijini kwa mtawanyiko wa umbali wa kilomita mbili badala ya kilomita moja kama ilivyokuwa hapo awali ili wananchi wengi vijijini wapate huduma ya umeme kupitia Taasisi ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Kauli hiyo ilitolewa Februari 15 na Waziri wa Nishati, January Makamba kwenye kikao cha kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ambapo aliwasilisha taarifa inayoanzia Januari 2021 hadi Februari 2022.

Baadhi ya Wajumbe wa Kamati hiyo walichangia taarifa hiyo ambapo walishauri namna bora ya kupunguza changamoto ya upatikanaji wa umeme nchini ikiwemo suala hilo la kusambaza umeme vijijini kwa mtawanyiko mkubwa zaidi.

Wajumbe hao waliongeza kuwa, Wizara ya Nishati isimamie pia miradi ya kufua umeme ya Mwalimu Julius Nyerere na Rusumo ili kupunguza changamoto ya ukosefu wa umeme wa uhakika nchini.

Waliitaka Serikali kutenga fedha ya kutosha ili kuweza kufanya ukarabati wa mitambo ya kuzalisha umeme na kusambaza katika maeneo mengi nchini.

Aidha waliishauri Serikali kupeleka wataalam nje ya nchi kwa ajili ya kujifunza namna bora ya kusimamia mitambo ya kufua umeme pamoja na kujifunza teknolojia mpya ya kufanya matengenezo bila kukata umeme.

Kuhusu upatikanaji wa umeme wa uhakika, Waziri Makamba alisema kuwa, uchakavu wa mitambo na miundombinu ya kusafirisha umeme ni chanzo kimojawapo cha kukatika kwa umeme mara kwa mara na hivyo kusababisha usumbufu kwa jamii.

Kuhusu mradi wa Bwawa la Nyerere, Waziri Makamba alisema kuwa, mradi huo kwa sasa unasimamiwa kwa ukaribu kwani lengo ni kuhakikisha kuwa unafanyika kwa ufanisi mkubwa.

# KATIBU MKUU NISHATI ATAKA WIZARA YA NISHATI IWE KITOVU CHA UFANISI

**Na Timotheo Mathayo, Morogoro**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba amewataka wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati kufanya kazi kwa uadilifu, ubunifu na weledi ili kuifanya Wizara ya Nishati kuwa kitovu cha ufanisi.

Mhandisi Mramba alitoa agizo hilo tarehe 07 Februari, 2022 wakati akihutubia Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati uliofanyika mjini Morogoro katika Ukumbi wa Ofisi za TAFORI.

Mha. Mramba alisema, Baraza la Wafanyakazi husaidia kuongeza tija na ufanisi wa taasisi pamoja na ushirikishwaji wa Wafanyakazi katika maamuzi ya pamoja mahala pa kazi.

Aliwajulisha wajumbe kuwa, mwajiri anao wajibu wa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu mahala pa kazi ili kuendelea kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa watumishi na kuongeza ari, ufanisiwa kazi, tija na na hivyo kuwezesha kufikia malengo yanayotarajiwa na taasisi.

Katibu Mkuu huyo wa Wizara ya Nishati, alisema, Watanzania wana matumaini makubwa katika kuona huduma katika Sekta ya Nishati zinaboreshwa ikiwemo upatikanaji umeme wa uhakika muda wote.

Alisema, Serikali inatekeleza miradi 17 ya kimkakati kati ya hiyo 7 inasimamiwa na Wizara ya Nishati ukiwemo mradi wa umeme wa Julius Nyerere.

Alibainisha kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, imeendelea kutoa fedha za kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo mradi wa umeme Julius Nyerere.

Aliwaasa wafanyakazi kutambua wajibu wao katika kazi badala ya kutanguliza maslahi binafsi kwa kuwa kila mmoja akitimiza wajibu wake, ufanisi utakuwepo na kupelekea malengo yaliyowekwa na Serikali katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati kufikiwa kwa wakati.




*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba akizungumza katika Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati lililofanyika mjini Morogoro tarehe 7 Februari 2022.*

Akijibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Mwenyekiti wa TUGHE, Wizara ya Nishati, Zghambo Chinula, Katibu Mkuu Mramba alisema kuwa, kwa kushirikiana na Menejimenti ya Wizara ya Nishati atahakikisha maslahi ya watumishi yanazingatiwa kwa kuweka mazingira mazuri ya kazi ambapo pia suala la uwajibikaji na kufanya kazi kwa kujituma na ubunifu ni mambo yatakayozingatiwa ili kuiwezesha Wizara kuyafikia malengo yaliyowekwa na Serikali.

Katibu Mkuu wa Nishati, aliwahimiza wafanyakazi wa Wizara na Taasisi zilizoko chini ya Wizara, kujiendeleza ili kupata ujuzi na maarifa yanayoendana na mabadiliko ya kiteknolojia ili kuleta matokeo mazuri katika kazi. Alisema, Wizara ya Nishati itaendelea kutoa programu za mafunzo kwa watumishi ili kuwaongezea ujuzi.

Awali Wajumbe wa Mkutano huo wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati, waliendesha zoezi la uchaguzi katika nafasi ya Katibu wa Baraza la Wafanyakazi ambapo Cosmas Kiguli

# KATIBU MKUU NISHATI ATAKA WIZARA YA NISHATI IWE KITOVU CHA UFANISI



*Mmoja wa wajumbe wa Mkutano wa baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati, Dorina Makaya akiuliza swali kwa mwezeshaji (hayumo pichani) wakati wa semina fupi kuhusu VVU, UVIKO na Magonjwa sugu yasiyoambikizwa iliyotolewa kwa Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati katika mkutano uliofanyika mkoani Morogoro tarehe 07 na 08 Mwezi Februari, 2022.*




*Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Wizara ya Nishati, Ziana Mlawa akizungumza wakati wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi uliofanyika mjini Morogoro.*

alichaguliwa kushika nafasi hiyo akifuatiwa na Fortutana Getere aliyechaguliwa kushika nafasi ya Katibu Msaidizi.

Katika mkutano huo wa siku mbili wa Baraza la Wafanyakazi, wajumbe walipatiwa fursa ya kujadili masuala mbalimbali ya kazi pamoja na kupewa elimu ya kukabiliana na ugonjwa wa covid.19 na kukabiliana na maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi pamoja na Elimu ya ujasiriamali .



*Wajumbe wa Mkutano wa baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa semina fupi kuhusu VVU, UVIKO na Magonjwa sugu yasiyoambikizwa iliyotolewa kwa Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati katika mkutano uliofanyika mkoani Morogoro tarehe 07 na 08 Mwezi Februari, 2022*

# WIZARA YA NISHATI NA DP WORLD YA DUBAI ZASAINI HATI YA MAKUBALIANO

Wizara ya Nishati na kampuni ya DP World ya Dubai zimesaini hati ya makubaliano ya ushirikiano katika kuendeleza miundombinu ya kupokea na kuhifadhia mafuta na gesi itakayojengwa nchini Tanzania.



*Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (kulia) na Mwenyekiti na Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya DP World ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bandari, Bohari na Eneo Huru la Kibiashara – Dubai, Sultan Ahmed Bin Sulayem (kushoto) wakiwa katika zoezi la kutia saini hati za makubaliano ya ushirikiano kuendeleza miundombinu ya kupokea na kuhifadhia mafuta na gesi itakayojengwa nchini Tanzania.*



*Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali (kulia) na Mwenyekiti na Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya DP World ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bandari, Bohari na Eneo Huru la Kibiashara – Dubai, Sultan Ahmed Bin Sulayem (kushoto) wakipongezana mara baada ya kutia saini hati za makubaliano ya ushirikiano kuendeleza miundombinu ya kupokea na kuhifadhia mafuta na gesi itakayojengwa nchini Tanzania.*

Utiaji saini huo umefanywa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali na Mwenyekiti na Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya DP World ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bandari, Bohari na Eneo Huru la Kibiashara – Dubai, Sultan Ahmed Bin Sulayem.

Mradi uliolengwa katika Hati ya Makubaliano husika ni kuendeleza miundombinu ya kitaifa iliyo bora na ya kisasa ya kupokea na kuhifadhi mafuta na gesi ambayo itatumika katika kuboresha sekta ya mafuta na gesi nchini na katika ukanda mzima wa Afrika Mashariki.

Tukio hili lilifanyika tarehe 27 Februari, 2022 katika Kikao cha Kibiashara kilichofanyika huko Dubai – Umoja wa Falme za Kiarabu.

# KATIBU MKUU NISHATI AFUNGA KIKAO CHA BARAZA LA WAFANYAKAZI

**Na Timotheo Mathayo, Morogoro.**

Baraza la wafanyakazi wa Wizara ya Nishati wamekutana kupitia masuala mbalimbali yanayowahusu watumishi ikiwa ni pamoja na kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya mwaka 2021/22 kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Januari, 2022.

Kikao hicho kilifanyika tarehe 7 na 8, Februari 2022, ambapo takribani Wajumbe 40, walijengewa uwezo kwa kupatiwa elimu juu ya kukabiliana na ugonjwa wa covid 19 na kukabiliana na maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi, Magonjwa yasiyoambikizwa, pamoja na ujasiriamali.

> **"kikao kingine kama hicho kitafanyika mwezi Machi, 2022 mjini Dodoma kwa lengo la kujadili mapendekezo ya rasimu ya bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka ujao wa fedha 2022/23."**

Kikao hicho cha siku mbili kilifungwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba.

Mhandisi Mramba alisema kikao kingine kama hicho kitafanyika mwezi Machi, 2022 mjini Dodoma kwa lengo la kujadili mapendekezo ya rasimu ya bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka ujao wa fedha 2022/23.

Alisema kuwa kikao cha maandalizi ya bajeti kinatakiwa kufanyika mapema kabla ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati kupitia na kuijadili rasmu hiyo ya mapendekezo ya bajeti.



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba akizungumza katika Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati lililofanyika mjini Morogoro tarehe 7 Februari 2022.*

# Naibu Waziri wa Nishati afanya ziara ya ukaguzi wa vituo vya kuzalisha umeme Ukerewe

**Na Timotheo Mathayo, Ukerewe.**

Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato amefanya ziara kukagua miradi ya umeme wa gridi ndogo (mini gridi) inayozalisha na kusambaza umeme katika kisiwa cha Ukara wilayani Ukerewe katika mkoa wa Mwanza.

Ziara hiyo imefanyika Februari 27, 2022 ambapo alikutana na wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Ukerewe na kupokea taarifa ya upatikanaji wa umeme katika wilaya hiyo.



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akisalimiana na kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya Ukerewe.*

Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Kanali Denisa Mwila alisema kuwa hali ya upatikanaji wa umeme wilayani humo imeimarika kutokana na matengenezo makubwa yaliyofanywa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Alisema kuwa, matengenezo hayo yalihusisha uwekaji wa waya wa majini pamoja na kusimika nguzo za chuma ndani ya eneo la Ziwa Viktoria kutoka wilaya ya Bunda mkoani Mara.

Kanali Mwila alisema kuwa, zipo baadhi ya changamoto ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa umeme Jua wa 3-phase unaotekelezwa na kampuni ya JUMEME katika maeneo ambayo




*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akikagua moja ya mashine za umeme jua (Solar) zinazomilikiwa na kusimamiwa na kampuni ya JUMEME yenye uwezo wa kuzalisha kilowati 180.*

# Naibu Waziri wa Nishati afanya ziara ya ukaguzi wa vituo vya kuzalisha umeme Ukerewe

hayajafikiwa na TANESCO.

"Kukosekana umeme wa uhakika katika baadhi ya maeneo inaongeza shida kwa wananchi pamoja na maeneo ya kutolea huduma za jamii kama shule na zahanati." alisema Kanali Mwila

"Kuna mazungumzo yaliyofanyika kati ya Serikali na uongozi wa kampuni ya JUMEME kuhusu suala la bei ya uniti moja kuuzwa kwa sh. 100 hadi 110, lakini bado kampuni haijakubaliana na bei hiyo kutokana na madai kwamba gharama za uendeshaji wa mitambo ya kufua umeme Jua ni ghali," amesema.

Meneja wa mradi huo uliopo kisiwa cha Ukara, Ahmad Rajabu alisema kabla Serikali kutangaza bei elekezi ya mauzo ya umeme kuuzwa kwa shilingi sh. 100, kampuni ilikuwa inauza uniti moja kwa sh. 3,500 kwa watumiaji wa majumbani.

Aidha kampuni hiyo ilikuwa inawauzia umeme wafanyabiashara kwa sh. 2,500 kwa uniti ambapo watumiaji wa viwandani waliuziwa kwa sh. 750 lakini baada ya Serikali kutoa bei elekezi, wenye viwanda wananunua uniti moja kwa sh. 375.

"Mradi wa Ukara unazalisha jumla ya kilowati 180 ambapo kituo cha Bwisa kinazalisha kilowati 60, Bukiko kilowati 60 na Chifule kilowati 60." Alisema Rajabu

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akihutubia wananchi, alisema lengo la ziara hiyo ni kukutana na wananchi ili kusikiliza maoni yao pamoja na wataalam kutoka kampuni ya kuzalisha umeme.

"Sisi kama Serikali tunakusanya maoni haya kutoka kwenu ili twende kuyafanyia kazi na hatimaye Serikali tuje na bei shirikishi itakayokuwa rafiki kati ya mwekezaji na watumiaji." alisema Byabato.

Wakati Serikali ikiendelea kulitafutia ufumbuzi suala hilo la bei ya umeme, Naibu Waziri ameitaka kampuni ya JUMEME iendelee kuuza umeme sh.100 kwa uniti moja.

Naibu Waziri alikagua mradi wa gridi ndogo 3 za umeme jua (Solar) zinazomilikiwa na kusimamiwa na kampuni ya JUMEME yenye uwezo wa kuzalisha kilowati 180 na mradi huo unahudumia wateja zaidi ya 2,500.

Alisema kuwa, maeneo ambayo hayajafikiwa na umeme ikiwemo baadhi ya vijiji na vitongoji vya Ukerewe yatapelekewa umeme, kwani Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuhakikisha maeneo yote nchini yanapata umeme wa uhakika ikiwemo kukamilika kwa mradi mkubwa wa Julius Nyerere.

Katika ziara hiyo Naibu Waziri alifuatana na wataalam kutoka EWURA,TANESCO, REA na wizara ya Nishati.



*Muonekano wa baadhi ya mitambo ya umeme jua inayomilikiwa na kampuni ya JUMEME, iliyopo Kisiwa cha Ukara- Ukerewe.*

**JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI**





***Fika Ofisi ya Mawasiliano,***
**Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au**
Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018
**Nukushi** +255-26-2320148

***www.nishati.go.tz***
***Wizara ya Nishati***
***@Nishati2017***
***wizara_ya_nishati_tanzania***
***Wizara ya Nishati***